MAELEZO YA UTANGULIZI YA MKURUGENZI MKUU MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI KATIKA HAFLA YA KUTOA LESENI YA HUDUMA ZA MAJISAFI NA MAJITAKA KWA MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA YA DODOMA (DUWASA)

25-05-2007

Mheshimiwa Patrick Rutabanzibwa, Katibu Mkuu, Wizara ya Maji; Bw. Simon F. Sayore, Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA;
Mhe. Balozi Job Lusinde, Mwenyekiti wa Bodi ya DUWASA;
Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la watumiaji Huduma;
Viongozi mbalimbali wa Wizara ya Maji;
Mwenyekiti wa Baraza la Serikali;
Menejimenti na wafanyakazi wa EWURA;
Eng. Peter Mokiwa, Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA;
Waandishi wa habari;
Wageni Waalikwa;
Mabibi na Mabwana.

Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, iliyo katika sura ya 414 ya sheria za Tanzania , inaipa EWURA majukumu kadhaa ikiwa ni pamoja na kutoa Leseni kwa watoa huduma katika sekta za Umeme, Mafuta ya Petroli, Gesi Asilia na Majisafi na Majitaka. Sheria hii inawataka watoa huduma wote katika sekta tajwa hapo juu kuomba na kupata Leseni kutoka EWURA kabla ya kuanza kutoa huduma kwa wale wanaoanza, au kuendelea kutoa huduma kwa wale ambao tayari wanafanya hivyo.

Ndugu Mgeni rasmi

Tangu ilipoanza shughuli zake rasmi Julai 2006 kufuatia uteuzi wa Bodi ya Wakurugenzi, EWURA imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kadhaa kama ilivyoainishwa katika ya Sheria husika katika suala la kupokea maombi na kutoa Leseni.

Katika sekta ya Majisafi na Majitaka EWURA inatoa Leseni kwa watoa huduma mbalimbali katika sekta hii. Kwa sasa, EWURA inatoa Leseni za muda (Provisional Licence) zikiwa na ukomo hadi mwezi Juni 2008 kwa mamlaka za makao makuu ya mikoa, na hadi mwezi Juni 2009 kwa mamlaka za makao makuu ya wilaya na miji midogo. Baada ya hapo, EWURA itaanza kutoa Leseni za kudumu (Permanent Licences). Leseni za muda zinatolewa tu baada ya mamlaka husika kukidhi baadhi ya vigezo vya kupata leseni ya kudumu. Muda uliowekwa kwa leseni za muda ni kwa ajili ya kuziwezesha mamlaka husika kuweza kukidhi vigezo vyote vya kupata leseni ya kudumu.

Ndugu Mgeni rasmi

Katika sekta ya Majisafi na Majitaka EWURA imekwisha pokea jumla ya maombi 19 kutoka kwa Mamlaka za Majisafi na Majitaka za miji mikuu ya mikoa na maombi 18 kutoka kwa Mamlaka za Majisafi na Majitaka za miji mikuu ya wilaya na miji midogo.

EWURA imeshapitia maombi yote za leseni ya mamlaka za miji mikuu ya mikoa. Kati ya maombi 19 mwombaji mmoja ametakiwa kuleta maombi yake upya baada ya kuonekana kwamba maombi yake yalikuwa na upungufu mkubwa. Waombaji 17 wametakiwa ama kurekebisha maombi yao au kuwasilisha nyaraka zinazokosekana ili kukidhi vigezo vya kupewa leseni ya muda. Mamlaka ya majisafi na majitaka, Dodoma (DUWASA) ndiyo mamlaka pekee iliyoweza

kutimiza vigezo vyote kwa ajili ya kupata leseni ya muda (Provisional Licence) mpaka sasa. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana kwa hilo.

Ndugu Mgeni rasmi

Mchakato wa kuomba na kupata Leseni kutoka EWURA unahusisha zoezi la kuchanganua maombi ya mwombaji ili kujua kama anakidhi vigezo muhimu kuhusiana na uwezo wake wa kiufundi na kifedha katika kutoa huduma husika. Mwombaji atapewa Leseni pale tu EWURA itakaporidhika kuwa, mwombaji anakidhi vigezo hivyo.

EWURA ilipokea maombi ya Leseni kutoka DUWASA tarehe 14 Machi 2007 na maombi yalifanyiwa uchunguzi wa awali kubaini kama DUWASA inakidhi vigezo vyote vya kisheria, kifedha na kiufundi kuweza kupata leseni ya muda. EWURA iligundua kukosekana kwa nyaraka kadhaa ambazo mwombaji alitakiwa kuleta na alifanya hivyo katika muda uliopangwa tofauti na mamlaka nyingine ambazo hazijakamilisha zoezi hilo.

Ndugu Mgeni rasmi,

Vigezo ambavyo inabidi vifikiwe ili mamlaka iweze kupata leseni ya muda ni kama ifuatavyo;

- Mamlaka iwepo kisheria, ijitegemee (autonomous) na iwe na Bodi inayosimamia shughuli zake kwa mujibu wa sheria.
- Mamlaka iwe na menejimenti na wafanyakazi wenye ufahamu wa kuweza kutekeleza majukumu yake.
- Mamlaka iwe na angalau hesabu za mwaka mmoja zilizokaguliwa (kwa mamlaka ambazo zilikwishaanza).

- Mamlaka iwe na mapato (mapato yake + ruzuku) ya kutosha kuweza kutoa huduma.
- Mamlaka iwasilishe mpango wa kibiashara (Business Plan) utakaopitishwa na EWURA.

Ili kuweza kupata leseni ya kudumu (permanent licence), mamlaka inapaswa ikidhi vigezo vifuatavyo;

- Mamlaka iwe na michoro na mpango wa matengenezo ya tahadhari ya miundombinu yake. (km. Mtambo wa kusafisha maji,mtandao wa mabomba,vituo vya kusukuma maji nk).
- Mamlaka iwe na hati miliki ya vyanzo vya maji pamoja na kibali cha kuchukua maji (water right).
- Mamlaka iwe na ripoti kuhusu hali ya kiuchumi ya jamii inayoihudumia (Social-Economic study report.
- Mamlaka iwe imetimiza masharti yote yaliyo kwenye leseni ya muda.

Ndugu Mgeni rasmi

Leseni kwa ujumla si kipande cha karatasi tu, bali ni nyaraka ya kisheria yenye kujumuisha haki na wajibu wa mpewa Leseni. Leseni hii inayotolewa leo kwa DUWASA inajumuisha mambo mengi, ambayo DUWASA itapaswa kuyazingatia. Lakini ningependa kutaja machache ambayo nadhani ni ya muhimu kama ifuatavyo:

Kwanza, leseni inasisitiza katika vifungu kadhaa umuhimu wa DUWASA kutoa huduma kwa wateja wake kwa kuzingatia sheria zote za nchi na maelekezo yeyote yatakayotolewa na EWURA.

Pili, utunzaji wa mazingira ni suala ambalo haliwezi kuangaliwa kwa wepesi linapokuja suala la kutoa huduma ya Majisafi na Majitaka. Ni dhahiri kuwa katika kutekeleza majukumu yake, DUWASA itajikuta

kwa kiasi kikubwa ikiingiliana na suala la utunzaji wa mazingira. Leseni hii inamtaka DUWASA kuzingatia suala la kutunza mazingira wakati ikitekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Leseni.

Tatu, Leseni inaitaka DUWASA kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za Majisafi na Majitaka kwa wakazi wote wa Manispaa ya Dodoma. Leseni hii inaitaka pia DUWASA kutoa taarifa mara moja kwa EWURA pale inapoonekana kuwa itashindwa kutoa huduma hiyo kama inavyotakiwa kwenye Leseni.

Nne, ni ukweli kwamba Leseni hii si zawadi ambayo mkiishapewa basi inakuwa yenu moja kwa moja na hivyo mnaweza kufanya lolote mtakalo.

Leseni hii inaweka bayana taratibu mbalimbali za kurekebisha mwenendo wa mtoa huduma pale asipozingatia maelekezo yaliyo kwenye leseni yanayolenga kuwa na huduma endelevu na yenye kujali maslahi ya wateja. Taratibu hizo ni kama vile, EWURA kuteua msimamizi wa shughuli za mtoa huduma badala ya Menejimenti yake, kuzuia mtoa huduma kuendelea kufanya shughuli fulani na hata kufuta Leseni.

Mwisho, Leseni hii inatolewa kwa DUWASA huku kukiwa na agizo la kuleta nyaraka mbalimbali kama zinavyoainisha na kwa utaratibu uliowekwa katika Leseni hii. Nyaraka hizo zinapaswa kuwasilishwa hadi kufikia mwezi Mei 2008 ikiwa ni kigezo mojawapo cha kuiwezesha DUWASA kupata leseni ya kudumu (Permanent Licence) ifikapo Julai 2008.

Ndugu Mgeni rasmi

Kama nilivyosema awali, EWURA inadhibiti pia huduma katika sekta za Umeme, Mafuta ya Petroli na Gesi Asilia. Utoaji wa Leseni umekuwa ukifanyika katika sekta hizo pia. Katika sekta ya Umeme, EWURA imetoa leseni za muda kwa makampuni mawili ambayo ni AG&P Power Ltd pamoja na Aggreko International Power Projects, yanayozalisha umeme kwa kutumia gesi asilia na kuuza kwa kampuni ya umeme Tanzania, yaani TANESCO. EWURA pia imepokea maombi ya leseni ya aina hii kutoka kwa kampuni nyingine mbili, APR Energy Ltd na Dowans Tanzania Ltd maombi ambayo bado yanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa upande wa sekta ya Petroli, EWURA imetuma kwa wadau wote wa sekta hii rasimu za Leseni zake mbili yaani, Petroleum Products (Wholesale) Licence na Petroleum Products (Retail) Licence kwa ajili ya kupata maoni yao. Wakati huohuo, EWURA inaendelea kufanya tathmini ya maombi ya leseni kutoka kwa watoaji wa huduma katika sekta hii na tunategemea kuanza kutoa leseni katika sekta hii ifikapo tarehe 1 Julai 2007.

Kwa upande wa sekta ya gesi asilia EWURA haijapokea maombi ya Leseni na watoa huduma katika eneo hili wanafanya shughuli zao kwa mujibu wa mikataba walioingia na Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) ambao ndiyo wenye leseni zilizotolewa na Wizara ya Madini na Nishati ambazo EWURA ina wajibu wa kusimamia utkelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika leseni hizo.

Ndugu Mgeni rasmi

Zoezi la kutoa leseni kwa watoa huduma katika sekta zilizo chini ya EWURA ni hatua kubwa kuelekea katika kuimarisha udhibiti wa

huduma katika sekta husika. Leseni zitakazotolewa, mathalani hii itakayotolewa leo kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka , Dodoma inajumuisha haki na wajibu wa mtoa huduma.

Ndugu Mgeni rasmi

Mwisho, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa DUWASA kwa ushirikiano walioutoa hadi sasa.
Pia ningependa kutoa changamoto kwa Mamlaka nyingine za Majisafi na Majitaka kuangalia hatua hii kama chachu kwa upande wao kuweza kufanikisha kupata Leseni kama DUWASA walivyofanya.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza